Hon Muthusi: Asante sana Commissioners. Maoni yangu mengi yamesemwa na wananchi na ninawashukuru sana, kwa hivyo nitaenda tu kwa haraka haraka kurudia. Kwanza ningependa kusema juu ya extension ya parliament. Sisi tunasema, Katiba iongezwe muda ifanye kazi pole pole kwa sababu hii ni Katiba tunayoitaka itumike kwa miaka mingi na hakuna haja ya kuharakisha kazi yenu. Kile kiko tu, mambo ya Katiba yasilinganishwe na muda wa bunge. Ikiwa bunge ni miaka mitano, wananchi wapatiwe jukumu la kufanya uchaguzi tena baada ya miaka mitano, ndio ikiwa wamechoka na wewe kama mbunge ama kama Councilor, wawe na uwezo wa kukuondoa. Kwa hivyo ninasema extension of parliament hatutaki.

Pili, ningependa kusema muda wa Rais ubaki ukiwa two terms. Ninakubaliana na wale wote waliotoa hayo maoni. Lingine tena ningependa kusema, pendekezo langu, pia muda wa wabunge ufanywe uwe two terms. Mbunge akiingia, asipotolewa akiingia mara nyingine hafai kugombea tena. Awapatie wengine nafasi pia nao wapate kuwahudumia wananchi, *ti kwikala vau mbaka ile wekwea vo*.

La tatu, ningependa kutoa maoni ya kusema ya kwamba, ni vizuri kabla ya uchaguzi wa Rais, iwe wale ambao wanaogombea urais waangaliwe akili zao. *Mukesa kusakua mundu wa nduuka*. Mtakuja kumchagua mtu na iwe kichwa chake si kizuri. So the sanity of the President is very, very important before we go for any Presidential elections. Hiyo ni safeguard.

Hayo mengine ni yale waliosema. Mambo ya masomo, tunataka Serikali itupatie free education. Kama vile tunavyojua sana sana pande za huku kwetu Ukambani, wazazi wengi wanataka kuwasomesha watoto na watoto wanataka kusoma lakini hatuna uwezo. Na ikiwa education ni free, ifanywe ya bure, ya bure kabisa. Si kusema ni ya bure halafu mzazi anaitishwa mia mbili yelo, sijui mia moja ya nini, tatu sijui ya kulia chakula. Hiyo haiwezekani. Ikiwa ni bure, ni bure. Ikiwa ni fees tuambiwe. *Yethiwa ni iana imwe*, tujue ni mia moja tutakuwa tukilipa.

Lile lingine ningependa kusema ni juu ya medication. Tupatiwe huduma za hospitali. Tuko na mahospitali mengi sana huku za Serikali lakini, zile pesa unazoitishwa ndio upate huo huduma, hatuwezi kuzipata. Na pili, hata katika hizo hospitali, hata madawa hakuna. Kwa hivyo Serikali iangalie health ya binadamu ama ya wananchi, iwe priority.

Lile lingine ningependa kusema ni juu ya constituencies, kule tunakowakilisha. Kuna constituencies zingine kubwa sana. Kama hii yangu ya Mutitu, ni kubwa sana, kubwa hata kushinda the Republic of Djibouti. Kwa sababu unaanza kutoka kule kwa lami mpaka kule Tana River. Tafadhali, tunataka constituencies zigawanywe ndio hata mbunge iwe yuko na uwezo wa ku-represent wale watu waliomtuma bunge lakini si kupatiwa pahali pakubwa ambapo maybe hautaweza kuwatumikia.

Katiba hii tunayoitengeneza, tafadhali iandikwe kwa lugha zote ndipo wananchi wapate kuijua. Kama vile tulivyo hapa, wengine

hawajui Katiba, wengine hawajaona Katiba na wengine hata hawajui Katiba inasema nini. Kwa hivyo Katiba iwe available na ipeanwe bure.

Lile lingine ningependa kusema ni huduma za machiefs. Napongeza yule mama alikuwa anasema machief wapigwe transfer. Ninakubaliana naye, lakini ningependa kuongezea. Hawa machief pia tupatiwe uwezo wa kuwapigia kura, wafanyiwe election. Kwa sababu machief wengine wanaingia hapo na wanaanza kutunyanyasa. Na wanatunyayansa kwa sababu wanajua hakuna njia ya kuwatoa. Lakini wakijua miaka ni mitano, tutawakaanga wasipotengeneza tabia. Kwa hivyo tunasema machief pia wachaguliwe.

Minimum election reforms. Mimi ninaona hiyo haifai. Ati tutengeneze sheria zingine za kuja kupiga kura, hapana. Kile tunataka, kwa sababu tunajua Rais Moi anaweza kugomea katika hiki kiti na kile tumesema ni two terms, aondoke, aondoke kabisa, *na athi yu*, kwa sababu tukisema hii Katiba iendeleo kucheleweshwa utaona mtu amekwamia hapo. Kwa hivyo vile Katiba inasema two terms na zake zimekwisha, iwe hivyo. Mambo ya minimum reforms hatutaki. Tumewakubalia sisi kama Wakenya mfanye kazi yenu na mtufanyie kazi mzuri na ya uaminifu. Vile munavyo tuamini na sisi tuwaamini.

Decentralization ya government funds. Pesa zinatoka kwa Serikali, tunapitisha kule bunge, lakini hizi pesa vile zinavyoteremka, zinaingia mifuko mingi sana ya watu. Zinaibiwa hapa kati kati. Tunataka pesa zinazopeanwa kwa Serikali, ziletwe mpaka kwa division. Watu wa division wakae chini, wapange vile wanataka kufanya na pesa zao. Sio wilaya zingine za Koibatek, zinapatiwa fifty million na zingine za Kitui zinapatiwa ten million. No! Zipeanwe kama zinatoshana na ziletwe huku chini wananchi pamoja na mbunge wao, pamoja na development committee wapange mipango yao.

Lile lingine ningependa kusema ni juu ya mambo tu ya elimu, ile bursary fund. Serikali huwa inapeana pesa za bursary, lakini wazazi wengi hawajui pale zinaenda. Tunasikia hizi pesa zinakuja tu katika mashule. Tunataka hizi pesa tuwe tukiambiwa, pesa zilizopeanwa zinapata kiwango fulani na committee ikae chini ijue watoto wale wa masikini wanaofaa kusaidiwa ni kina nani. Kwa sababu iko magendo nyingi sana. Pesa zinakuja za bursary na mshemiwa anaandika majina ya watoto wake, ama mwalimu anaandika majina ya watoto wake. Hiyo hatutaki. Lazima katika Board wawe wanajua ni pesa ngapi na zisaidie wale ambao hawajiwezi.

Domestic violence. Hii ni mambo ya kutwanga kina mama. Mambo hii ya bill ya kupigana hata tulikuwa nayo bunge lakini makosa watu wanadhania ni kama kina mama ndio upigwa tu. Hapa kuna wanaume wamenyamaza pia hutwangwa, *ukwa ni kuweta tutawetaa. Ve aume vaa makunawa muno ni iveti syo.* Kwa hivyo tukisema domestic violence tunasema violence, either kwa mama ama kwa baba. Na kuna violence ya aina nyingi. Kuna vitu kama rape, *tikukindana, kikamba.* Mama ama msichana anashikwa kwa nguvu na akienda police station anasikia haya. Kwanza, kitu cha kwanza askari anakuuliza *wekindawa ukeka ata?* Si unaona utaogopa? Na kuna magonjwa, labda huyo mtu amekupatia nini... hata ugonjwa mbaya. Kwa hivyo tungependa pendekezo la, tuwe na special police desk ya kina mama ama ya wanaume ya

kupeana mambo yao private, si pale katika counter, kama mtu ame najisiwa.

Lile lingine ni kupeana pesa kwa vyama vya kisiasa, political parties. Pendekezo langu, political parties zipatiwe pesa baada ya uchaguzi, sio kabla. Ndio, ikiwa muko na 5% ya viti vya bunge mpatiwe. Tukisema tupatiwe kabla, kila mtu ataanza political party yake na bibi yake, *na akyasa ndunenge mbesa*, kwa sababu niko na nini, niko na chama. Kwa hivyo zipeanwe kwa uwezo ama nguvu, the strength in parliament na katika percentage ya vile walivyoingia.

Village elders, wale *atoi*. Tunapendekeza, hawa *watoi* wanasaidia D.O. na ndio wanasaidia chief, ndio wanasaidia assistant chiefs. Hawa 'watoi' wachukuliwe na Serikali, wawe wakilipwa mishahara. Kwa sababu bila kulipwa mishahara ndio wanatugonga sana na kutuitisha *usoo*. Na hiyo *usoo* inakuwa nyingi sana. Kwa hivyo tunataka wawe wakipatiwa mishahara, ndio tuwe tukijua vile tutakuwa tuki-deal na hiyo mambo yao ya *usoo*.

Defection, kuhama chama kuenda chama kingine. Hii inagharimu Serikali pesa nyingi sana kufanya uchaguzi. Mimi ninapendekeza, ikiwa hauwezi kuvumilia miaka mitano katika kile chama kilichokupeleka bunge na unataka kwenda hapa katikati, iwe kuna fine ama pesa kiwango fulani kimewekwa upeane kwa Serikali. Serikali, hatuwezi kubali iwe ati leo umepigiwa kura, unaenda unauza kura za watu, unaruka chama chako halafu Serikali inatukia pesa tena kufanya uchaguzi. It is very costly. Kwa hivyo lazima tutafute sheria ile itaweza, ya kusimamisha hayo mambo ya kumangamanga, kwa kisiasa.

Serikali ya mseto, kama vile ilivyosemekana. Serikali ya mseto itatusaidia sana kwa sababu, saa zile watu wanapigania uongozi, wanataka kusaidia nchi yetu ya Kenya, na ikiwa chama fulani kimeingiza wabunge fulani na kingine wabunge fulani, ni lazima Serikali ijue hawa wabunge wamepatiwa mamlaka na wananchi. Na ikiwa wanagawanya wizara, pia hao wawe-considered kupatiwa wizara ndio wafanye kazi tuinue nchi yetu ya Jamuhuri ya Kenya.

Nguvu za Rais, mtukufu Rais. Nguvu za mtukufu Rais, yeyote atakaye kuwa, Daniel Moi ama Muthusi Kitonga. Ni lazima nguvu za Rais zikatwe, kwa sababu hata siku hizi tunasema Rais anapatiwa mamlaka ya kuwachagua mabalozi, ya kuwachagua ma-judge. Hivi vitu tunataka pawe... if it is the Parliamentary Commission or Judicial Service Commission ifanye recommendation, recommendation iletwe parliament, parliament ikubali, President atangaze, lakini sio kitu mtu kufanya kienyeji na ati peke yake.

Ningependa kuuliza, Katiba inasema Rais akifariki makamu wa Rais anashikilia kwa muda wa ninety days. Hiyo ninaona ikiwa na shaka kidogo. Kwa sababu ukipatiwa ninety days ushikilie, kukutoa hapo ni ngumu sana. Ukinipatia ninety days, hauwezi kuning'oa. Sasa, pendekezo langu, ningependa Speaker wa bunge ashikilie baada ya kifo cha Rais, na wakati wa muda huo wa ninety days, uchaguzi uitwe wa Rais na Speaker asiwe mgobeaji, ndio iwe fair play.

La mwisho ningependa kuuliza, Katiba yetu iangalie hizi korti, makorti ya kusikiliza cases. Kama huku pande ya kwetu korti

iko tu Kitui. Ukitoka hapa kuenda kortini lazima utoke leo ikiwa kesi yako ni ya kesho, na ikiisha kesho utarudi kesho kutwa. Kwa hivyo tungependa, hata ikiwa korti haziwezi kujengwa, tuwe na mobile courts. Iwe mkuu wa sheria na Chief Justice wameangalia mobile courts ya kutembelea pahali fulani na kusikiliza maswala ya wananchi juu ya kesi zao, ndio kuwapunguzia gharama.

La mwisho kabisa, ningependa wakati wa uchaguzi, vyama vyote ama wote wanaogomebea viti vya u-president ama bunge wapatiwe fair ground. Hakuna kutumia State machinery. Ati wewe unakuja na gari za G.K. kuomba kura. Ikiwa kura zimeitanwa, vile Charity Ngilu ataenda na gari yake, na wewe tumia yako. Vile Kibaki ataenda na gari yake, Moi atumie yake, lakini si kutumia mafuta ya Serikali, D.O. wa Serikali, ndege ya Serikali na *mwolio* wa Serikali. *Mwolio* ni ile mahindi tunapatiwa bure wakati wa kura. Kwa hivyo tupatiwe fair playing ground. Na la mwisho kabisa ndio Councilor tusigombane naye, muwaongeze macouncilor mshahara, haki wanaumia sana. Asante sana.

(Clarification) **Com Wambua:** Just a... Mheshimiwa tafadhali kidogo. I think some clarifications. Mine is very short. You talked of two terms, two terms, two term. MPs to have two terms, the President two terms but you never said for how long. Is it five years, four years two years?

Hon Muthusi: I meant two terms of five years each.

Com Wambua: Of five years, okay, for record purposes.

Com Mosonik: Mheshimiwa ukasema kuhusu hizo defections. Ukasema wale wanataka kuhama chama wapigwe faini lakini ningependa kuuliza kuhusu wale ambao wamekihama chama kifikara na kwa kusema wazi lakini wanasema wanakaa tu kwa kile chama cha zamani, technically ndio wasipigwe faini ama kupigiwa kura tena. The ones who are in a different party practically but they are technically remaining in the old parties to avoid what you are suggesting.

Hon Muthusi: Hiyo itakuwa ngumu, kwa sababu hivyo ulivyo sema ni penzi la roho, na penzi la roho si kutenda. Lakini kuandika barua ya kujiuzulu umetenda. Saa hii labda sitasimama na SDP, lakini hiyo si kusema nimekihama kwa sababu hakuna uchaguzi utafanywa juu ya kusema hivyo.

Com Wambua: Asante sana mheshimiwa, nafikiria maoni yako tumeyapokea na tutayaangalia tutayachunguza tuya...

Hon Muthusi: Asante sana.

Com Wambua: Asante sana, thank you very much. Tafadhali jandikishe huko. Beatrice Kalenga, tafadhali. Lugha, utatumia gani?

Beatrice Kalenga: Kiswahili.

Com Wambua: Kiswahili, haya endelea mama.

Beatrice Kalenga: Asante sana, hiyo ni maajabu sana kwa vile hayo yote nilikuwa nimepanga ni kama yamesemwa lakini... Hiyo ya kwanza nilikuwa na maoni juu ya maombi ama worship. Siku hizi tunaona kuna makanisa ama dini nyingi zinazoendelea. Lakini kwa vile kuna mwenzangu mwingine aliongea juu ya hiyo, mimi yangu ni kusema kama inawezekana hiyo worship iwe allowed lakini hiyo ya devil worshippers... kwa sababu hata tukiangalia sana hiyo ndio inaleta corruption, inaleta tofauti tofauti katika watu wa Kenya hiyo iwe banned kabisa.

La pili ni, tulikuwa tunasikia mambo ya rape cases in Mutitu. Lakini siku hizi tume-witness hiyo. Sasa hiyo nilikuwa ninasema, hata kuna mwingine amesema, huyo mtu ama the rapist akipatika apatiwe life sentence. Asiuwawe ndio akisikie. Kwa hivyo akifungwa maisha ndipo atajua amefanya makosa ana hiyo ndio ninaomba Katiba kama watapitisha, wapitisha hiyo iwe ni life sentence.

Lile lingine ni, vile tunasikia watoto wetu. Siku hizi marriage imekuwa sio marriage, imekuwa ni tukae, 'come-we stay'. Nilikuwa ninaomba kama kuna njia inawezekana mwanamke na mwanamume wakikaa pamoja angalao wawe na kitu cha kuwatambulisha ati sisi tumeona lakini sio kukaa hivyo hivyo kwa sababu, atakaa siku mbili tatu ama miaka kumi na baada ya mwanamume kuona mwanamke ako na watoto ishirini anamtoroka, anamwachia huo mzigo. Sasa ningeomba kama hiyo Katiba itakayotengenezwa, itatengeneza at least kitu cha kuonyesha, hawa watu wawe na kibali cha kuonyesha kuwa wameoana lakini sio kuachwa hivyo. Kwa sababu wanawake ndio wataumia, mtu anaachiwa mzigo na hana baba, watoto hawana baba au nani mwingine wa kumsaidia. Na ndio unaona kuna watoto wengi yaani hawa street children. Na hayo ndio yalikuwa maoni yangu. Kwa majina ni Beatrice Kalenga.

Com Wambua: Asante sana mama, jiandikishe hapa tafadhali. Tunataka kumwita Gideon Mwakavi.

Gideon Mwakavi: Asante sana Bwana Chairman wa Commission, group yako na MP, D.O., chief na wazee wengine. Ninajua nyote mko wazima. Maoni yangu ni kama matatu hivi. La kwanza ninachangia maoni yangu kuhusu mashirika kadha ya kiserikali.

Kwanza, nitaanza na National Social Security Fund, hilo shirika bwana Commissioner, nimeona imewasumbua wafanyikazi sana. Kuna mapesa ya watu yamekwamia kwa hiyo shirika ya National Social Security Fund. Ningeomba hilo shirika lenu ama Commission hii, ichunguze juu ya kwamba kuna hii sheria iliyowekwa kama hujamaliza miaka kama hamsini na tano huwezi kulipwa hiyo pesa. Kuna watu wengine wameretire, wengine wameachishwa kazi na ukienda kwa hilo shirika unaambiwa

huwezi kupatiwa pesa kabla ya kufikisha hiyo miaka hamsini na tano. Kwa hivyo ningeliza, hilo shirika tafadhali commission mpunguze hiyo miaka na iwekwe kama mtu aki-retire apatiwe pesa yake kwa sababu ikikaa pale hakuna kazi inamfanyia.

Pia, kuna wengine wanakufa kabla hawajapatiwa hiyo pesa. Unamwacha mke wako, pia naye anakufa, anawaacha watoto lakini ni wadogo hawajafikisha miaka ya ku-claim. Ningeliza huo mswada upunguzwe kidogo, iwe kama ni mtoto na ana-guardian, huyu guardian awe anaweza kufuata hiyo pesa ya huyu mzee ambaye alikufa halafu huyu mtoto apatiwe kitu cha kumsaidia.

Bado kwa hiyo hiyo National Social Security fund. Kuna huyo employer ambaye amekuandika na anakata mshahara wako anaupoleka kwa National Social Security Fund, lakini haufiki, hizo pesa haziendi huko. Utakuta mtu ame-claim, na pia akipelekwa hiyo statement utakuta miezi kadhaa hakuna ama miaka fulani hakuna hiyo pesa. Ningeliza hiyo Commission iangalie, hiyo nimeona ni kweli. Hiyo pesa ambayo tajiri hakupeleka zilienda wapi na mtu ame-claim anaambiwa utapatiwa hiki na kile kingine utaongojea. Kwa hivyo tumeona mwananchi anataabika akiwa ame-retire na ikiwezekana hiyo shirika ipunguze sheria zake.

La pili, ninaenda kwa national Hospital Insurance Fund. National Hospital Insurance Fund, imekuwa kama watu wengine wamekuwa wakitoa pesa kwa hilo shirika na wakaambiwa labda utapatiwa kibali cha kuenda hospitalini utibiwe bure, wakulipe bure nini... Lakini hadi wa leo hizo pesa zinaenda kwa hilo shirika, hakuna chochote mtu akiwa mgonjwa analipiwa. Hizo pesa zinakaa pale kama miaka ishirini... ningeliza hii Commission iangalia, hizo pesa ambazo mtu amekatawa kwa miaka hii yote, kama anaweza kurudishiwa kwa sababu hakuna kazi zimefanya huko. Zinakaa tu, zinarudikwa kule. Wengine wanafaidika na wengine hawafaidiki. Kwa hivyo ningeliza Commission iangalie hiyo kwa sababu watu wengine wanaumia sana.

La tatu na la mwisho ni mishahara. Watu wengi wanaumia sana, bwana Commissioner kwa hiyo mishahara. Mtu anaanza kwa kupata elfu mbili, mwingine anaanza na elfu moja mia tano na ukiwangalia ana watoto, kama ni wazee wana bibi, na kumbe huo mshahara, duka ile tunaenda na mtu wa elfu ishirini ndipo huyu mtu anaenda kununua chakula pale.

Kwa hivyo ninaonelea ya kwamba, the Review Commission ifanye mshahara wa chini kama shilingi elfu kumi, ili mwananchi ambaye atapata kazi awe angaa anaweza kuwalea watoto wake na pia jamaa wake kwa njia mzuri. Anaweza kununua nguo, kuwapatia mahitaji ya kutosha badala ya kupatiwa shilingi elfu moja au elfu mbili ambazo haziwezi kumsaidia na duka ni ile ile tu ambayo inauzwa vile vitu vya thamana.

Na kwa hayo machache Review Commission chairman, nimesema asante sana na hayo ndio maoni yangu.

Com Wambua: Asante sana Bwana Gideon, ujiandikishe huko. Tumwite Joram Kamuli, halafu atafuatwa na Councilor Joseph Siengo, kama yuko.

Joram Kamuli: Kwa majina ningetaka kusema ni kama vile tu mumeyasikia ni Joram Musavi Kamuli. I would like to talk more about the disabled people as far as this Constitution is concerned.

First, we are asked in this Constitution changing that, the mechanism of the government... There is a question asking whether there is any mechanism that the government should put into place to ensure maximum participation in the governance by the persons with disabilities. I would like to answer that question and then forward my grievance s to the new Constitution.

The government should create job opportunities for the educated lame people. Why? For example, like myself I think everybody can see that I am lame or rather that I am disabled. I have tried to secure employment in those big towns like Nairobi, Mombasa, and whenever I go anywhere that there are employment opportunities we assemble with so many other men. Whenever the Personnel manager checks me and he notices that I am disabled and that the heavy duties done there I cannot do, that automatically renders me unsuitable and I am disqualified from that work.

My plea is, may the government or the new Constitution that we are looking forward to, look into the lame people and create salaried job opportunities for them to be absorbed into, maybe in the offices. Because for example, you may find somebody is educated, he can do the office work and although he is able to do such work there are no vacancies for him/her to work.

The nomination of councilors should also include those people with disabilities. With the present Constitution, we could hear that some people are being nominated, some MPs are being nominated but we have not seen anybody with disabilities being nominated.

Schools for the physically or the mentally handicapped should be started for them to be educated like the other people, so as to meet the cost of all the human needs. Loans should be given to the handicapped or the priority to get loans from banks to continue with our businesses like the way other people do.

Mobility, the lame people either physically or mentally should be given the priority to move from one place to another either by being given a certain card by the government or by being introduced or by the public notice to the vehicle owners from the government nationwide, so as for them to move from the place they come from to the place they would like to cater for their needs.

The income per capita as we have seen, the lame people, we have said that whenever we talk of the income per capita in every budget reading, we should be given or the income per capita should allow everybody working or non-working to get at least 5% of Kenya's money when it comes to the time of budgeting.

Judiciary; All Kenyans should be educated more about all the laws of Kenya so as not to suffer the consequences of not knowing. That is to mean that, there is no need for me to walk during the night time only to meet a policeman who tells me that I am not walking at the right time and I have not seen anywhere written that I should not be walking at a certain time. So, we should be given all the laws or rather the law should be taught to everybody so that we can be knowing what is wrong and what is not wrong. It is quoted that “*Where there is no law, there is no mistake...*” Unless I know the law, I think there is no mistake for me to be told I am doing something wrong.

There is this other thing, whenever we are trying to uplift our lives... For example I can become a hawker in a market and you find these Council people coming to collect all the goods that I am selling there. You find that I am left... I went to that market to sell my goods so that I can get at least something to cater for my needs and then you find that those goods have been taken. Now, where am I to go? Now, it means that I should go the offices of the Council so that I can get back my goods and when I go there, I may be told to give at least Kshs 4,000, of which is very unfair to me and I remain without my goods that I got through very difficult circumstances.

We have heard a lot about the geographical constituencies that they should remain the way they were before. To us, we find this not to be good. For example, if we could talk more about this constituency of Kitui Eastern. We have said that the constituency should have the common characteristics, socialism and communication. Why? Because you cannot imagine somebody from Kitui ginnery bearing the same constituency with somebody from Malalani. Whenever that person will be talking or will be forwarding his grievances to the government or to his delegates about the scarcity of water that person from ginnery. When somebody from Malalani is telling the delegate that we lack water, somebody from...

(Interjection) **Com Wambua:** Kamuli tafadhali malizia malizia...

Joram Kamuli: Nitamaliza maliza, kidogo tu.

Com Wambua: Umemaliza dakika kumi lakini nitakuongeza ingine moja.

Joram Kamuli: Moja, tafadhali asanti sana. Sasa tungetaka hii constituency iwe inagawanywa na iwe ni kidogo, iwe ni ya watu ambao wanaelewana na wana shida moja si kama vile ilivyo. Asanteni sana.

Com Wambua: Thank you very much Bwana Joram, tafadhali jilandikishe pale. Councilor Joseph Siengo. Councilor tutakupa dakika kumi kama wale wazee wengine mbele yako kwa hivyo mulika tu yale ya muhimu halafu utuambie, utatumia lugha gani?

Cllr Joseph Siengo: English.

Com Wambua: English, okay carry on please.

Cllr Joseph Siengo: My name is Joseph Siengo, Councilor Mutitu ward, Kitui County Council. I wish to take this opportunity to present my following views. I will start with the issue of land. I would like to state that all title deeds issued by the Commissioner of Lands should be freehold rather than on lease. We know currently we have both, the lease and the freehold. This should only apply in cases where a third party utilizes the land on agreement with the owner and the agreement signed before a lawyer.

(End of tape)

Should the government or any other party want to utilize such a freehold land for activities such as conservation of animals or mining, compensation of the land should be based on the value of the activity being undertaken, rather than the government value of the land in the district. If the activity is for example, mining of gold, the value of the land should be higher than when soda ash is being mined.

Due to the importance attached to land in this country, let there be established a Land Law Court of Appeal to deal with the last stages of land cases rather than the present situation where their views are made to the minister of lands. Anybody handling land cases at any stage should have some knowledge of the Land Act.

The Commissioner of Lands should be appointed by parliament and be given security tenure of office for a period not exceeding ten years and be answerable to the same parliament that has appointed him.

My next item is on remuneration of parliamentary and civic leaders. I am very happy Honourable Commissioners that my Member of Parliament has hinted on this. I would like to say that all the parliamentary and civic leaders are elected by the public and are both responsible in developing their electors, in one way or the other. Although the parliamentarians represent the public in a larger area called the constituency and are more responsible than the civic leaders who represent a ward that does not warrant the big gap between their monthly remuneration.

It is pathetic, Commissioners that what a Councilor earns in his total five years term is equivalent to what a member of parliament earns in one month. To make matters worse, their paymasters are different despite the fact that the two serve the same people. While the parliamentarians are paid through the Central government budget, the civic leaders are paid by their Local Authorities and at rates given by the Central government based on the financial strength of the individual Local Authority.

Commissioners, almost 90% of the Local Authorities in Kenya are basically poor and pay between Kshs 7,000 and Kshs. 10,000 per month as compared to the payment of almost a million paid to the members of parliament monthly.

In order to narrow this gap, I propose that the civic leaders be paid from the Central government budget like the members of parliament or from the consolidated fund. I also propose that a body of Commission be established or the current electoral Commission of Kenya be given the responsibility of paying both leaders at reasonable difference. This will encourage professionals and better-educated people to join civic leadership, bringing quality leadership both to the Council and their wards of representation.

Honourable Commissioners, yesterday or the day before yesterday I did give views on behalf of the Council. I feel... that was in Central and the views held here in the Eastern Kitui. I wish just to touch a bit on what we said as a Council.

We said we should have a government where we have a President as the Head of State and a Prime Minister as the Head of the Government. We should have a Central Government with autonomous Local Government system as the basis of decentralization. There should be established a District Council in every district.

The District Council should be headed by a chairman who should be elected by inhabitants of district council through a secret ballot. To be eligible for elections, as chairman, one should be thirty-five years of age, the standard of education be ordinary level that is Form IV and above. A local resident of the district and a person of high integrity. There should be a code of conduct for all civic leaders and officers of the Local Government.

There should be an established national Local Government assembly to oversee the operations and formulate policy guidelines for Local Government. The National Local Government Assembly should be composed of all the District Council chairmen.

We should have an established Local Government Service Commission which shall have power to appoint Local Government officers. For one to qualify for elections as a Councilor, he should be of acceptable level of education. Nomination of Councilors should be limited to special interest groups.

No person should be a chairman for more than two, five-year terms and the Council should only be dissolved after the expiry of the five years term. And here I would clarify that the District Council we are talking of has the same boundaries as the County Councils we have currently. With that Commissioner, ladies and gentlemen I wish to stop there.

(Clarification) **Com Wambua:** Thank you very much Councilor Siengo but there is one question from the Commissioner.

Com Raiji: Councilor Siengo, you have touched on an issue that 90% of the Local Authorities do not have sufficient funds to remunerate Councilors. Isn't it also a fact that they also do not have resources to develop the areas of their jurisdiction, and what would you say as to the common criticism that some of these institutions, wards and districts are unviable and that in fact

they should be abolished because they have become a burden to the people as we have heard people claiming that cesses are too high.

As a Councilor what would you say to that, because that is one of the issues that was raised here that you are charging too much to the locals because obviously there you do not have sufficient revenue pays to meet even the salaries of the Councilors leave alone the development of the areas under your jurisdiction?

Cllr Siengo: Honourable Commissioner, my suggestion that the Councils should have an overload of the payment of the Councilors that is the government should take care of the payment of the councilors. That will enable the Council retain some amount of money and possibly it would be possible to lower the rates or the cesses.

I have also pointed out that all land be freehold. By that I if a member of the public has a piece of land here or a plot and it is freehold, he owns it so there would be no rates paid for it. But if it is a lease like it is today, you will be required to pay some rates to the Council or to a body like... or even to the government. My suggestion is, the Councils should have an offload of part of their activities, part of their expenses like paying the councilors.

Com Wambua: Asante sana Councilor Siengo, tumepokea maoni yako kwa hivyo jiandikishe hapo, halafu tumuite John Mauta Tama, atafuatwa na Livai Kilonzo. Livai Kilonzo awetayari. Tafadhali Mauta, tutakupatia muda wa dakika kumi utupatie maoni yako. Taja jina kwanza halafu uendelee.

John Mauta Tama: Jina langu ninaitwa John Mauta Tama na niko hapa nikiwa kama mzee wa miaka yote nikiwa hapa. Ninataka niseme maneno ya miaka karibu nane hivi iliyokwisha. Kunacho kitu kimoja tuna taabu nacho, hiki ni kazi. Kazi zinatusumbua sana watu wengine. Tuna watoto lakini hawapati kazi, tunaambiwa hakuna kazi. Serikali ikituambia hakuna kazi, tunaenda wapi? Hiyo ni neno moja.

La pili, miaka karibu tano au kumi hivi tumekuwa na chief mmoja anaitwa Monyo. Amechukua watu hapa Mutitu Location akawaandikisha askari tano polisi, akawaandikisha askari tano wa military kwa division sita. Je, Serikali hiyo ilienda wapi? Okay, tunataka kujua ya kwamba kama inawezekana kuandika watu military, police, Kenya Army GSU kama iko kuandikwa tupeane authority kutoka Mutitu Location, kwa sababu huku ni msituni. Hii nyumba ni sisi tunajenga, kwa sababu huku ni msituni na chief hawako karibu na sisi. Na tunaambiwa sisi ni watu wa Mutitu wa Kitui, Kitui ni wapi?

Hiyo kazi ikija kupeanwa hapa hatumtaki MP hapa, hatutaki Councilor hapa kwa sababu ataendewa usiku aambiwe maneno mengine, mengine, mengine aje achukue mtu asiye faa kazi awache yule anafaa kazi kwa nini? Hapa, hawa wawe mbali. Akiwa hapa ni shauri yake tu atajua vile atakaa na watu wake sio ninamwambia aondoke hapa kwake.

Kitu kingine, tunaambiwa hakuna kazi na tuna mahali sana ya kazi. Tupewe ‘malakita’ sita, watupatie misitu ya kulima mashamba ya kulima mashamba ya Serikali. Serikali itaenda kutuuzia hii chakula sisi wale watu tunashugulikia hiyo shamba. Hata Kiambu si kuna mashamba? Kwani kwetu hakuwezi kuwa mashamba ya Serikali? Kwani tuna nini na mchanga ni moja? Hakuna mchanga ingine. Kwa hivyo tafadhali ikiwa Serikali inaangalia taabu za watu.

Kuna nafasi zingine tunanyimwa zikiwa ni zetu. Kuna mtu anaweza kukosa kazi kwa kuwa hajui kusoma. Kuna watoto ambao tuko nao na wanajua kusoma lakini kazi zimewakosa na mtu akiwa na degree ati anakosa kazi. Sasa atasoma aende wapi? Tunashindwa hapo kabisa na ni watoto wetu. Watoto wa watu wengine kama Kitui town, unajua ni watu wako karibu na D.C. na D.C anauwezo, wakienda wanasema andika huyu, andika huyu, kwanza ile kazi iko... anaandikwa saa hii hii tu. Mimi ni mfanyikazi ninajua mambo ya sheria ya kikazi.

Kwa hivyo sasa tafadhali, tusaidiwe kwa njia iliyofaa. Tuletewe polisi hapa. Tilitangaziwa polisi waletwe hapa na ni mimi nimeongea na Chief Kitonga na akanipa chupa nne, (Inaudible) tukinywa pombe. Nikamuuliza wewe wale watoto wetu ambao ni wangwana watandikwa kazi ya polisi wakitoka wapi na wewe uko hapa... iko watu wanaandikwa Kitui, iko watu wanaandikwa Kitui. Kitui, D.C. analala na wale watu, walikuwa ni watoto wao. Wakitaka kazi basi... Na D.C asubuhi yake ni kupeana kazi, enda uandike huyu. Na wale watu wakuandikana wale wanatoka (inaudible) wako na watu wao kufika huku wako na ndugu zao walipokeana nao wakanywa pombe mpaka asubuhi. Asubuhi hakuna kuandika watu, ni kuitwa majina tu kwa sababu yaliandikwa usiku wakinywa pombe.

Sasa mambo kama hayo, tusaidiwe tafadhali, tusaidiwe na Serikali. Si ati tusaidiwe na mtu, tusaidiwe na Serikali ikiwa ni yetu. Mtu ukipeanwa yuko hapo, akiitishwa yuko hapo. Tafadhali, mimi ninaitwa John Mauta Tama, musikaninsahau mimi.

Com Wambua: Tumesikia mzee tunakuhakikishia maneno yako tumeyapokea tutayapeleka Nairobi, kwa hivyo kama huna cha kuongezea, tumpe mwingine nafasi.

John Mauta Tama: Kwa hivyo, kwa kuongezea, kuhusu polisi tukazaniwe ndio...

Com Wambua: Hiyo ya polisi imeingia tayari.

John Mauta Tama: Imeingia tayari. kuna nyingine moja tafadhali. Hospitali. Mimi nimelala njiani nikija huku Mutitu na hospitali iko hapa Mutitu juu, nayo kuikanyaja ni shilingi ishirini. Sina pesa, nitaikanyaga namna gani? Na kutibiwa ule ugonjwa ninao ninatakiwa nilipe shilingi mia moja. Kama sina shilingi ishirini, mia moja nitapata wapi?

Kwa hivyo sasa, tusongeshewe hospitali ya kutusaidia. Tukiumwa na nyoka, tutakufia huko huko, hakuna dawa. Asante.

Com Wambua: Asante sana Mzee Tama, jiandikishe hapa tafadhali. Livai Kilonzo.

Speaker (from the audience): (inaudible).

Com Wambua: Utamsomea memorandum? Kwa hivyo ufanye vile vile ulivyofanya. Taja jina lako na utaje unamsomea nani memorandum.

Celestine Maanzo (reading on behalf of Mr. Livai): Asante, ninaitwa Celestine Maanzo, ninasoma memorandum ya Mr. Livai ambaye ni elder, Mutui, Kaayo Village, Manyoeni sub-Location in Kaliku Location. Their recommendations are as follows:-

They recommend that women remain under men because that is what God said. Two, they recommend that the Constitution be translated in all languages for everyone to know what it says. Three, they recommend that the President's powers be reduced and he should not be above the law.

Four, they recommend that the President should have only one term of five year, no more no less. Five, they recommend that the government should take care of the aged, either in a home or finance their up-keep from wherever they are. Thank you.

Com Wambua: Asante sana, tafadhali jiandikishe hapa kwa niaba ya Kilonzo Livai. Tumuite Michael Kasanga.

Michael Kasanga: Hamjambo. Mimi nina mambo kadha. Kwanza...

(Interjection) **Com Wambua:** Taja jina kwanza liingie kwa microphone.

Michael Kasanga: Mimi ninaitwa Michael Kiima Kasamba.

Com Wambua: Kasamba.

Michael Kasamba: Ningependa kuanza na quota system. Quota system ni motion ambayo iliwekwa na Martin Shikuku karibu miaka kumi iliyopita. Na hii quota system ni uandikaji wa watu katika kazi za Serikali na Parastatal bodies. Lakini ina walakini. Iianza vizuri lakini sasa ikawa inageuzwa kama biashara.

Kwa mfano hapa kwetu Kitui, wakati watu wanapoandikwa kazi kama waalimu ama watoto kuchukuliwa kwenda university maana yake hiyo unapata katika quota system. Watoto wetu wengi wanaachwa kwenda university, kwa sababu wanachukuliwa watoto wengine kutoka nje, wanajaza nafasi zao kwa sababu ya pesa. Yule aliye na pesa nyingi, mtoto wake

ndiye atachukuliwa. Na kwa uhakika hata mjumbe wa area hii anajua watoto wetu ambao wako katika university kutoka constituency hii ni wachache sana. Na hii inakuja through quota system.

Kwa hivyo, mimi ninaomba kwamba, hii quota system ipigwe marufuku na isifanye kazi tena. Turudie mtindo ule wa zamani. Yule ambaye anasoma vizuri, anapita vizuri, aende university bila kuwa na matatizo yoyote.

Kuandikwa kazi, watu waandikwe katika tarafa sio katika district. Kwa sababu ikiwa kama ni kazi ya polisi ama army ama kazi nyingine yoyote, watu wanaandikiwa katika Kitui district kama hapa kwetu. Na hapa watu kama kutoka kule Malalani amabao unasikia (?), pesa ni kidogo. Si siri, mapato yetu yako chini sana. Watu wale ambao walio na uwezo waweze kufika Kitui na matangazo yanakuja kama siku mbili namna hiyo kwa sababu inafunikwa watoto wa wenyewe waandikwe.

La pili ni retirement kwa member wa parliament. Watu ambao tunawachagua kwa kura, wanatufanya sisi ni kama tuwaabudu kama ni sisi waliotuandika na hii ningependa iondolewe. Iwe wajumbe wanajua kuwa watu walio wachajua kwa kura ndio mabwana wao. Kwa sababu ikiwa mtu anaingia katika bunge, yeye hakuandikwa na Serikali, alichaguliwa na wananchi. Alichaguliwa na wananchi kwa kura na hakuandikwa katika kipande na haifai apewe pension.

Pension iondolewe kwa wajumbe, kwa sababu wanapata mishahara mikubwa sana halafu wakishafanya kazi kwa miaka mitano, ile proposal yao waliweka katika parliament walipwe pension, hata sio miaka kumi, miaka tano, na wewe hukuandikwa, amefanya kazi gani kwa wananchi? Amewafanyia watu nini na yeye anaenda kule kupata pesa? Hiyo kwa maoni yangu ninaona, iondolewe wasipate pension. Ya pili hapo hapo, yaani (b) yake, mishahara yao ni mikubwa sana ipunguzwe.

Majimbo; Unajua hapa kuna sehemu mbili ya watu ambao wanataka majimbo na wengine wanataka Central government moja. Mimi kwa upande wangu, ninapinga majimbo. Iwe ni Serikali moja, na President mmoja.

La nne limesemwa na mimi nitalisema tena, ni NHIF (National Hospital Insurance Fund). Watu wengine wamefanya kazi kama miaka hamsini na haja enda hospitali hata siku moja, na bibi yake ama watoto wake. Na amepewa retire na ile pesa inapotea kwa Serikali, kwa nini? Hii pesa inafaa irudishiwe mwenyewe akitoka ikiwa hajazitumia. Hiyo ni mali yake.

Elimu; kwa wajumbe. Elimu kwa mjumbe iwe ni Form IV mzuri ama awe amejijenga na ni mwanasiasa mzuri ambaye anaweza kuchaguliwa kuenda bunge. Na President, elimu yake iwe ni ana degree yaani ni graduate.

La tano, watu walio-retire kutoka kwa Serikali na Parastatal bodies, ile pension wakati watu wanaongezewa kwa Serikali ama wakati President anapenda ama bunge inapooonelea kama watu hawa inafaa waongezewe, watu wote, na wao vile vile

waongezewe mishahara, waongezewe mishahara yao, waongezewe katika pension yao.

La sita ni juu ya ma-Councilors. Elimu ya ma-Councilor nimesikia inakuja Form IV, na mimi nina swali. Je, kuna watu ambao wamefika Standard Eight ambao ni wazuri sana katika County Council na nchi yetu haijaendelea sana bado iko nyuma sana. Mimi ninaonelea ma-Councilor elimu yao iwe ni Standard Eight. Na hayo ndio maoni yangu, wananchi na ma-Commissioner, asante sana.

Com Wambua: Asante sana mzee, tafadhali jiandikishe pale. John Mutemi, halafu atafuatwa na Joseph Kiteme.

John Mutemi: Thank you very much Mr. Commissioner. I am going to talk about the issue of the Electoral process in this country. The issuance of voter's cards and the IDs, to me they mean one and the same thing. Every Kenyan today over the age of eighteen is eligible to have a voter's card, is eligible to have an ID. If you have an ID, to me you are eligible to vote. The issue of voter's cards is just to manipulate the electoral process. You are a Kenyan citizen, you have the ID, you have to vote.

President's powers over the EC, the Electoral Commission. The Chairman of the Electoral Commission is appointed by the President, I think we are all well aware of that, and all its members. This means that the President elect or the President who appointed the Chairman has powers over the Chairman and can sack him, so the Chairman would play to the tune of the President.

Kenyan living abroad... point number three, we are very much aware that they do not vote. I do not know why and they are Kenyans. I do not know why the government is scared to let them vote, they sell them their franchise... this is somewhere I would propose that the government should be very keen on. Majority of these votes from outside can change the election results in this country. We believe most of the people who reside outside are well educated, they still have ties with their families and I do not see any reason why they should be denied that Constitutional right.

On the issue of education, I would beg to differ with most of the speakers here, who said that MPs, Councilors, the President, maybe should have attained a certain amount of education. It is not mandatory that if you are intelligent or if you have education you have wisdom, no. Education should not bar. Leadership comes from God. Winston Churchill, the most celebrated Prime Minister of Britain, never had a university degree but he led Britain to prosperity.

About the system of government, I propose the parliamentary system of government whereby, the Prime Minister is the Head of the Government and the President, head of State. I propose a cabinet, which shall be responsible to the legislature. I propose that the appointment which shall be done by the President, who is just the Head of State to be vetted by parliament. I concur with a speaker who said that the ministers should not only be members of parliament, but they can be members from the public who are skilled in particular fields.

Lastly, but not the least of course. I would propose for an independent judicial system in Kenya. A system whereby judges who are appointed and vetted by parliament are not responsible to any other person apart from parliament and they can work and execute what they have been appointed to do without fear. Thank you very much.

Com Wambua: Bwana Mutemi, what do you do with yourself?

John Mutemi: I am a lawyer.

Com Wambua: A lawyer, there is a question.

Com Raiji: Did I get you right that you are proposing that there be no academic qualification for candidates for any of the posts of Councilor, President and MPs? If so, are you advocating even total illiteracy, and if that be the case how will these candidates be able to read the Constitution, Standing Orders or even newspapers?

John Mutemi: Thank you Mr. Commissioner. I say this because I believe that I am in a democratic State where we are not going to vet somebody just because of his intelligence academically. This is a free society, where a person should elect a person of his choice regardless of ethnicity, creed or whatsoever or even education.

I do not advocate for illiteracy, Sir, but I would like to see democracy being exercised at its fullest. We are not going to treat education as a disability or inability to perform. Thank you.

Com Wambua: We do not want to debate, but these two concepts are contradictory. If you do not advocate for illiteracy, then you definitely advocate for a minimum education, which you are also saying, should not be there. So, anyway, we do not want to open a debate, but it would appear to us that there is an element of contradiction.

John Mutemi: Thank you.

Com Mosonik: There is one on the ID being adequate for voting purposes, I wanted to ask whether it matters where an individual votes, whether it is in a ward or in a constituency or not? And if it does, how do you identify voters in terms of their area?

John Mutemi: Okay, thank you very much. I previously talked about the IDs. I prefer that if a Kenyan has an identity card, the card stipulates where you have been born, your division, your whatever. That is the only area where you should vote. Only that.

Com Wambua: I would thank you because you have avoided to comment on the other issue, but thank you very much for your contributions Bwana Mutemi. Please register yourself there. Let us have Joseph N Kiteme.

Joseph N Kiteme: Thank you. I am Joseph Nzula Kiteme and these are my views as far as the Constitutional Review process is concerned. Since Kenyans or rather citizens of Kenya have been given this responsibility to give out their views, I do propose that our Constitution should have an identity or what we call the Preamble.

As far as the three arms of the government are concerned, I do propose that parliament, the executive and the judiciary to be independent of each other. This is because when we look at the executive it is as if it controls the other arms of the State.

On the powers of the executive, I do propose that they should be limited. For example you cannot, under the current Constitution prosecute the President for any criminal or civil offences and yet he is just a person or a citizen like us.

Since Kenya is a signatory of the Universal Declaration of Human Rights, the Constitution, which we have, does not clearly show the structure for implementing the Bill of rights. Therefore, I do propose that the Constitution to show clearly how the Bill of Rights will be implemented.

The current Constitution does not also address the socio-economic human rights and the environmental and development rights. Therefore, I do propose that those issues of socio-economic human rights and the environmental and development right to be looked at.

I also propose that a Constitutional office for the Ombudsman to be established. Since in Kenya there are some people who are not able financially and since they cannot fend for themselves they need some people or an office where they can forward their problems and get help. I propose for a special office to be established to look into Constitutional issues. For example, right now in front of us, we have a Commission, which has been established for the Constitutional Review Process.

Since we have contributed towards this process of making a new Constitution, I also propose that when there is need for amendment, the citizens should be consulted. With those few points I wish to stop there.

Com Wambua: Thank you very much for your views, please register yourself there. Let us have Justus Musyoka. Taja jina lako mzee na uendelee. Utatumia lugha gani?

Justus Musyoka: Kiswahili, lakini nita-mix na Kiingereza.

Com Wambua: Uta mix na Kiingereza?

Justus Musyoka: Ndio.

Com Wambua: Haya sawa endelea.

Justus Musyoka: Asante sana. Jina langu ninaitwa Justus Muthengi Musyoka. Kwa maoni yangu kama mzee ni kwamba...

(Interjection) **Com Wambua:** Is it Justus or Joseph?

Justus Musyoka: Justus.

Com Wambua: Justus...

Justus Musyoka: Justus Muthengi Musyoka.

Com Wambua: Okay.

Justus Musyoka: Ikiwa tunataka kuwa na Serikali ambayo ni very strong na very effective, mimi nina-propose ya kwamba lazima tuwe na head of State ambaye ni President wa hiyo Serikali na pia tuwe na Prime Minister, kwa maoni yangu, sio Vice President lakini Prime Minister.

President atakuwa na mamlaka yake tofauti na yale ya Prime Minister. Prime Minister, mimi ninafikiria kwa maoni yangu ya kwamba, atakuwa aki-run the affairs of parliament na policies of the government. Na ikiwa kuna swali lolote ambalo lina ugumu kwake awe aki consult the President ili watafute suluhisho.

Pia, lazima kwa maoni yangu, ninaona ya kwamba Speaker wa bunge achaguliwe na wanabunge lakini kutoka ile party ruling party ambayo imezidi kwa kutengeneza Serikali. Na huyu Speaker wa bunge awe impartial, asiwe akipendelea wanabunge kwa sababu ametoka kwa chama hiki na hataki wanabunge wa chama kile. Awe impartial kabisa.

Pamoja na hayo, opposition parties in any given country, ikiwa kama mfano hapa Kenya tuko na opposition parties na ruling party. Wale ambao ni sitting, ambao ni... kwa mfano kama Speaker wa bunge awe akiwaona wote ni sawa. Sio awaone kama wa opposition parties ni enemies. Kwa jumla ni kusema ya kwamba, wa opposition parties wawe wakionekana kama ni watu ambao wamechaguliwa na wananchi, waende wakatengeneze sheria huko na wanahitaji heshima. Kwa hivyo ni lazima waheshimiwe, wasionekane kama enemies.

Pia na kwa upande wa opposition parties nao, pia wao wasione kama sitting government ambayo ni the sitting ruling party, wawewakiwaona kama ni enemies, hapana. Wawe wakiwaona kama hao ni brothers and sisters kwa kutengeneza sheria za nchi, ili wakiona mambo au policies za government zingine wasizipinge kama ni kwa sababu ni wao wabunge wanapinga, wanapinga, wanapinga, ili waone failure ya sitting ruling party, hapana. Wawaunge mkono kwa policies zile ambazo zinaenda sambamba vizuri na wananchi.

Kwa sababu wakiziheshimu zile policies za sitting government although ni wapinzani, wataenedelea na kuuza ule upinzani wao kwa raia na eventually raia watakuja kuwapenda na pengine next time wataweza kuchukua nafasi ya userikali.

Kwa hivyo, maoni yangu ni kwamba, wa opposition in any given country kama hapa Kenya lazima wawe wakiheshimiwa na wao waheshimu ile sitting government. Na kwa hayo machache Bwana Chairman, ninakomea hapo. Asante sana.

(Clarification) **Com Wambua:** Kidogo tafadhali Bwana Justus...

Justus Musyoka: Yes...

Com Wambua: Mimi ninaona kuna shida kidogo. Ulisema Speaker awe elected by MPs kutoka kwa...

(Interjection) **Justus Musyoka:** Parliament, kutoka kwa the ruling party, ile ambayo...

Com Wambua: The ruling party?

Justus Musyoka: Ndio, ile ambayo imekuja kwa power...

Com Wambua: Haya, halafu ukaendelea ukasema awe impartial...

Justus Musyoka: Yes, akiwa Speaker sasa, a-vacate kile kiti chake kama MP, sababu akiwa hapo, anything that comes there, atakuwa akipendelea kwa upande ule wake. Lakini akiwa impartial, atakuwa akifanya kama huku Mutitu ataona kama kwa Bwana Muthusi, kunahitajika kitu fulani anapeana kwa Muthusi, anapeana kwa yule mwingine, if possible. Lakini sio kusema kwa sababu yeye anapendelea pande moja, ya kule ametoka.

Com Wambua: Okay, kwa hivyo atachaguliwa from sitting MPs but to vacate his seat as soon as he is...

Justus Musyoka: Yes. The same thing like what happened to Speaker Fred Martin...

Com Wambua: Sawa, sawa. Asante sana, jiandikishe hapa tafadhali. Tutamwita Rebecca Kamonde, halafu atafuatwa na Steven Makau. Mama utatumia lugha gani? (in vernacular).

Rebecca Kamonde: Ma-officers wa Serikali, kutoka kwa MP wetu, D.O wetu, councilor wetu, mabibi na mabwana hamjambo?

Response from the audience: Hatujambo.

Rebecca Kamonde: Ningependa kusema ya kwamba, Serikali hii tumeweka Katiba siku ya leo, Katiba ya nchi yetu ya Kenya na kutoka mwaka wa 1978, 1979, Serikali, Katiba ya Kenya ilikuwa inaendesha Serikali vizuri sana. na wakati huu tumefika mwaka wa 1996, mabadiliko yakaanza kutokea katika nchi yetu ya Kenya. kwa sababu tuliona watu wanaanza kuambiwa waache kazi. Watu wengi wa Kenya wakaacha kazi na wakaondoka wakaambiwa mtapatiwa shilingi elfu mia moja na hizi pesa walizitumia zikamalika, na hawa watoto wana watoto shuleni. Na haya mabadiliko yakaleta wivu sana hapa katika nchi hii ya Kenya.

Jambo lingine ni kwamba hii hospitali yetu haina pahali pa kuweka dawa ya nyoka karibu na watu. Kutoka hospitali ya karibu hapa Mutitu hata nyinyi ma-officer wa Serikali munapitia hiyo njia munaona matope mengi huko njiani. Kwanza hii njia gari ikiondoka hapa asubuhi saa kumi, mtu akiwa mgonjwa hawezi kuenda Kitui. Hatuna gari ya hospitali hii yetu, hata mtu anaweza kufia hapo hapo.

Watu waliotoka kazi mwaka wa 1996, hawajapokea mapato yao, hiyo pesa yao ya NSSF mpaka sasa. Waliambiwa wamalize miaka hamsini na tukifika mwaka wa elfu mbili, watoto wengine wakaandikwa kama hawa. Na mwaka huu ukimalizika hawa watoto watafukuzwa. Unaambiwa wanafukuzwa na mzungu anayeitwa Leakey. Je hiyo kamati yetu ya Kenya itatutuma tumchague President ambaye haendeshi nchi hii yetu vizuri. Tunataka maendeleo mazuri hapa nchini Kenya.

Lingine ni kuhusu hapa Mutitu. Hapa Mutitu kuna mlima ambao unafaida kubwa sana. una maji na tuliambiwa kuwa huo mlima wa Mutitu umeuzwa, umeuzwa na nani? Hatujui ni nani ameuzwa. Kwanza ninataka huyo MP wetu au Serikali yetu ambayo ni kamati yetu tuliyochagua tuende tuandike, tuungane na Serikali yetu kujenga huo mlima tuzuie maji mengi ili tupande mboga, na tuone ndege zimetoka London zimekuja kuchukua mboga hapa kwetu Mutitu. Ndio tuone mapato ya watoto wetu. Ni hayo tu, nimeshukuru sana.

Com Wambua: Na huu mlima, nani ameuzwa, umenunuliwa na nani? Unajua?

Rebecca Kamonde: Tumesikia kuwa huu mlima unauzwa, kutoka kwa watu hapa Mutomo, kutoka kwa watu wanaopiga

piga midomo hapa bure wakisema mlima umeuzwa na wakati wa zamani huo mlima ulikuwa unafanyiwa kazi na watu hamsini na sasa hawa watu wamefukuzwa wakaenda. Sasa huo mlima hauna wafanyikazi sasa. Basi simwaandike watoto wetu ambao wamemaliza form IV, mtu wa class cha nane waanze kufanya hii kazi kama miaka ya 1990.

Com Wambua: Kwa hivyo wewe hujui na huna hakika, unasikia tu.

Rebecca Kamondi: Ninaona tu muendele kufanya tu hiyo kamati yetu ya Kenya tuanze kuandika watoto wetu.

Com Wambua: Asante sana mama, jiandikishe hapo tafadhali. Steven Makau yuko wapi? Na sasa bwana Makau ndiye atakuwa wetu wa mwisho.

Steven Makau: Honourable Commissioners, my name is Steven Makau and I am presenting my personal views based on some points in the Constitution. Number one, I propose that our government should have a way of assisting the young and especially the orphans, the very aged and the destitutes who are always in problems and have nobody to assist them in the country, and also those who are physically impaired.

I also propose that our government should have very strict anti corruption laws where those involved in corruption are severely punished. We should also have fair and unified national distribution of resources where, development in all districts and in all divisions takes place almost at the same range. You will not be surprised in our country to find out that some of our provinces or districts being very much advanced while others lag behind and lack very essential facilities. My proposal is that national, development should be unified and especially as concerns facilities of essence.

I also propose that the President should not have powers over the judiciary and over parliament. He should not be the one appointing senior officers in these lines, there should be Boards to do that. Presidential powers to dissolve parliament and even to give pardon in cases that have been decided in court should be cancelled, as this shows that he has powers over parliament and even powers over our courts.

There should be constitutionally formed commissions and Boards that should appoint and dismiss senior government officers and not the President. These boards, should include the clergy and other people of high integrity in the country.

I also propose that government salary scales should not be as they are today, where some people are getting millions when others are suffering. I propose that, the difference between the highest salary and the lowest should not be more than two hundred times as is the case today. The difference between the lowest and the highest is more than a thousand times. It should be something between... something less than two hundred times. I also propose one man, one job in the civil service.

The Constitution should also be set to control the misuse of public funds. As is the case today, some funds in the government are misused and nothing or nobody takes action about it. I also propose that, remuneration of parliamentarians should be recommended by a separate and independent body and not the same people discussing and recommending their salaries.

I also propose that our national President should not be a party President and should love and cover all political parties in his speeches and not only his party because his journeys, his allowances and his expenses as a President are met by the consolidated fund.

I also propose that, there is no need for nominated MPs as they only come there to serve those who nominated them and not the interests of the nation. I also propose that misuse of land and the environment should be punishable by law. There should be laws to enforce and to check on things like soil-erosion controls, and provision of health facilities and misuse of environment, especially pollution. These should be checked through the Constitutional laws as they spread diseases to the citizens.

I also propose that there should be compulsory, free primary education and free medical services to all people of Kenya. Lastly, I propose that there should be occupation accountability, a kind of report for every mature citizen whereby every citizen is issued with the kind of Identity Card or certificate to show what he does in the country and what he produces in a year. There should be some kind of a check to make sure that everyone is involved in doing something beneficial, something productive and this has to be recorded and be reported every year. This one will minimize vagrancy, thuggery, idleness and poverty in the country where people just sit idle, idling about throughout yet they eat/consume food daily. Everyone should be productive in the country. With that, I would like to say thank you.

Com Wambua: Asante sana, there is one clarification, just hold on.

(Clarification) **Com Mosonik:** It is on the question of this Commission on appointments and dismissals and you said you involve the clergy I would like to ask you the question, how do you relate that to the idea, that the State and the church should be separate that “you give unto Caesar the things that are Caesar’s and to God those which are His” secondly, whether also the State should be involved in hiring and firing in the church?

Steven Makau: Thank you. The State has always been involved in the church because it has been interfering with the churchmen when they mess about. They are fired and even taken out of the country. The State has always been having power over the clergy, controlling them and even firing some priests and some clergymen when maybe they say things that do not please them. The State has always been having power over the clergy. But what I am saying is this...

Com Mosonik: Let me not argue with you. You know what, we are making proposals...

Steven Makau: Yes, I am proposing this...

Com Mosonik: Just listen, please, about a new Constitutional dispensation okay. We are saying let us write a Constitution which will guide us to live in the future and to live better. So we do not say since the State has been interfering with the church all this time, we give up or we say therefore the church must interfere with the State.

I was just asking, the question of the secular and the sacred, the church and the State being separate, how do you address that in the light of your recommendation and secondly whether we should also write it in the Constitution, the right of the State to interfere in the church or church affairs?

Steven Makau: Thank you. First I wanted to say that the right of the State is there interfering with the church, the right is there, because we belong to the State and the State is ours and the church gets permission to come and preach to the people of Kenya from the State.

What I was proposing and I am proposing is that, for important and very important commissions that should appoint senior officers like the Attorney General, the Chief Justice, the Auditor General, the Chairman of your Commission and these senior people, they should not be appointed by an individual, seated at a desk and saying I appoint Mr. Makau, I appoint Mr. Cheriyot, no. It should be appointed by a board and I am proposing that this board should be composed of people with integrity.

Like the Board can consist of a Bishop from CPK, a senior man in the government, a person from a non-governmental organization, these high ranking people that are people of integrity. But not just one person seated at a desk and when he is annoyed by someone or at someone who made a remark the other day, he is fired the following day.

I mean, I am saying that somebody should not be given all those powers to behave, as he wants. People of integrity should do the work.

Com Wambua: We have noted the point so thank you very much for your contribution, please register yourself on that desk. Mary Nzinga?

Celestine Maanzo: I have a memorandum.

Com Wambua: Come and read it in the usual way. Give us your name and indicate whom you are reading it for.

Celestine Maanzo: Thank you I am reading a... I am Celestine Maanzo, I am reading a memorandum for Ushirika Wa

Wanawake Wa Kristo, A.I.C Manyoeni in Kaliku Location, Mutitu Constituency. The issues they have highlighted are domestic violence, property rights, bad culture, rape against girls, women and disabled women.

For the first one, they recommend that domestic violence should end forthwith. The second one, they have recommended that they should have equal property rights with or as their spouses. Three, they have recommended that the Constitution should do away with bad cultures, for example, circumcision of women. Four, they have recommended that rape against girls, women and disabled women should carry the highest penalty that is death. Thank you.

Com Wambua: Asante sana kwa hiyo memorandum ya Mary Nzinga. Tutamwita Kituku Kasea, halafu atafuatwa na Raphael Mwakavi. Kituku Kasea, lugha gani?

Kituko Kasea: Ya Kiswahili.

Com Wambua: Haya. Taja majina na uendeleo.

Kituko Kasea: Jina langu ni John Kituku Kasea. Mimi nimezaliwa hapa Kitoo Sub-Location, Kitoo Village, Mutitu Location, Mutitu Division. Mimi, hata na baba yangu wamezaliwa hapa. Lakini ninasikitika sana kwa vile mambo yakitoka juu, yakija chini huwa yame-change. Kwa mfano, ningependa kabisa, sheria, kila mtu awe chini ya sheria lakini sio sheria iwe chini ya mtu. Kwa mfano, kama vile tulivyo sasa kuna majeshi yako mikononi mwa mtu mmoja, korti iko mikononi mwa mtu mmoja na hata mahali popote hapo tukisema kweli ni mikononi mwa mtu mmoja.

Yaani ninaposema mikononi mwa mtu mmoja nina maana kwamba kila mtu hata kutoka President, yaani Rais mpaka hata na mtoto mdogo wawe chini ya sheria lakini sio mmoja apite mbele ya sheria.

La pili kama vile inasemekana ya kwamba ati land iwe mikononi mwa mtu fulani ambaye yeye ametoka. Nikitumia hiyo neno hata kama kuna mtu wa Mombasa hapa asije akanikasirikia. Ametoka Mombasa kuja hapa. Ukipambana na yeye kweli, ukiwa uko na vitu vinono, yaani pesa, bila shaka shamba litakuwa lako na huyu hata aseme nini, hatakubaliwa hiyo shamba na hiyo korti ndio ninauliza kama ingetolewa kwa Land Commission na iletwe kwa ukoo yaani 'mbai', hiyo ingekuwa bora.

Kitu kingine ni, wakati Serikali ilipokuwa ikiundwa, I mean, tukinyakuwa uhuru wetu, tulikuwa tukiambiwa umasikini utakwisha, ujinga utakwisha, magonjwa yatakwisha. Sasa, hayo mambo yote, kila kitu kinazidi kunona, kutumaliza sisi. Ujinga, unatoa pesa. Hata kama mwalimu anapata mshahara lakini kuna ile inaitwa tuition. Sasa hiyo ati anataka hiyo ndio watoto wapite sawa sawa. Na hii inatokana na akitaka promotion, atakwenda huko juu, sijui ni wapi, sio mbinguni lakini atakwenda kuwaona boss wake wale wakubwa wako huko juu. Na hii promotion upende usipende ataipata.

Haya mambo ya ujinga sasa hii inaanza kuja, watoto chokoraa wanaanza kuwa wengi. Hiyo ndiyo njia moja ya kujaza chokoraa huku. Na pia, ikiwa mimi ni mzee na niko na shamba na nikiambiwa shamba si langu na nimenyanganywa na pesa, nikifukuzwa, pengine niko na watoto ishirini. Sasa hiyo ina-support chokoraa wazidi kuwa wengi.

Kitu kingine, ni hili jambo wanasema ati magonjwa yamalizike. Yatamalizika namna gani na ukienda huko hospitali, unaambiwa kwanza kukanyaga hayo mawe yenyewe ya hospitali, kuyakanyaga namna hiyo, toa pesa, shilingi ishirini. Kukanyaga tu, peke yake, na ukishindwa na hiyo ishirini wewe uende nyumbani. Sasa tunamaliza magonjwa ama tunayaongeza? Hiyo sheria nayo inazidi.

Lingine ni haya mambo ya kusema...

(Interjection) **Com Wambua:** Mzee tupatie mapendekezo pia. Unataka tufanyeje? Ndio tuandike yale mapendekezo yale unataka tu.

Kituko Kasea: Kama vile mapendekezo yangu ni kwamba, ningependa tu, kila mtu, Mkenya yeyote awe chini ya sheria. Land Board iwe kwa ukoo, lakini si kupea uwezo mtu mwingine, hiyo ndio pendekezo langu. Lingine ni haya mambo ya hospitali, kwa maana mtu anaweza kuwa akifa na ukakosa shilingi ishirini unafukuzwa, anakwenda na anakufia njiani. Hata hiyo statement sijui utaandika namna gani. Sasa hiyo, ningependa ukiingia hospitali basi umeokoka. Kama bahati yako ni mbaya huyu mtu atapona, kama ni bahati yako mbaya atakwenda mbinguni. Hicho ni kitu kingine kimoja.

Kuhusu hii habari ya maskini, inaonyesha kuwa hawa masikini wameanza kuzaa sana. Kwa maoni yangu, vile mimi ninaona, watu wa nje, ninafanya kusikia na redio tu na pengine Kiswahili kina ponyoka ponyoka, lakini ninasikia ati parliament, parliament... ajabu! Parliament yenyewe, mjumbe anapata nusu million. Na akipata nusu million, mimi sina kitu, sina kazi, watoto wangu hawana kazi, wengine wako na degree, hawana kazi. Sasa hii yote wewe unayakua, na nyingine inaongezwa traveling allowance and so forth...

Ningependa hiyo mishahara ya wabunge iwe kama, afadhali iwe kama kitu kama elfu mia moja, afadhali hiyo kidogo. Lakini sio kunyakua hizo pesa zote. (*Laughing from the audience*) Sasa wakinyakua, wanaanza ku-blame Serikali, Serikali haina kitu... Wewe uko na ngapi? Wacha Serikali, umanyakua ngapi? Sasa haya mambo, kwa maoni yangu ninaona kama ni kupora tu. Wanapora Serikali inakuwa haina kitu. Basi hapo ndipo nilikuwa ninasema kwamba wakati mwingine mimi ninaona pengine member of parliament hapana zunguka, zunguka hivi, hapa hatumwoni.

Ningeuliza kama ingewezekana hafanyi kazi kutosheka yaani wananchi hawatosheki, angalao akae miaka mitatu tu, na baadaye tupewe nafasi ya kumchagua mwingine. Akimaliza hii tano, sisi tunaumia, hata nyinyi mumeona barabara hapa iko namna gani? Mumeumia. Kwa hivyo, ninauliza nafasi tupewe ya mjumbe akimaliza miaka miwili ya tatu anakwenda.

Com Wambua: Haya Mzee asante sana. tumeyasikia maoni yako kwa hivyo jiadikishe hapo tafadhali. Mwakavi? Haya kuja hapa tafadhali, lugha?

Raphael Mwakavi: Asante sana Bwana Mwenyekiti, asante sana, kwa kunipatia hii nafasi, na asante sana kwenu kwa kuja kwetu kuyachukua maoni kuhusu utekelezaji wa Katiba ya sasa ambayo itatekelezwa kutoka kwa maoni ya wananchi. Mmefanya vizuri sana. Maneno yangu ambayo ninataka kusema ni machache, ambayo wakati huu nimekaa hapa tangu asubuhi nimejaribu kusikiliza lakini kuna mambo yamerukwa ambayo ni shida kwa wananchi.

Jambo la kwanza ningependa kuzungumza ni juu ya ofisi ya D.O. Ofisi ya D.O. kwa mfano, sisi hapa Mutitu tunapakana na Wasomali na wanaweza kutuvamia wakati wowote, na hata hivi sasa wanaweza kutuvamia, kwa sababu wako hapa karibu Endau. Lakini Bwana D.O. wetu hana simu, hana gari, hata sanduku la posta hakuna. Tukivamiwa sasa, sisi sote tutakimbilia milimani kujificha. Kwa hivyo, iwe sheria, popote Kenya ambapo kuna D.O. awe na gari, simu yake isiwe ikiharibika, na hata awe na Sanduku la Posta. Hiyo iwe sheria. Na mimi ninajua hiyo ni sheria ijapokuwa imevunjwa.

La pili, hospitali. Jambo hili limezungumziwa sana lakini kuna shida ya hospitali ambayo haikuguzwa. Hapo zamani, hospitali zilikuwa na magari, kulikuwa na dereva wa kuwapeleka wagonjwa katika hospitali kuu. Lakini kwa sasa kuna magonjwa mengine yanasababishwa na wadudu, kwa mfano, kuumwa na nyoka, mbwa wa kichaa. Unapowapeleka hospitalini ambayo ni health center hapa Mutitu, unaambiwa uwapeleke Kitui na magari yetu hapa Mutitu yanaondoka saa kumi na moja. Sasa ukiambiwa uwapeleke Kitui utawapeleka na nini? Inabidi ungoje mpaka kesho, na huyu mtu anakufa. Mimi ninajua hiyo ilikuwa sheria na imevunjwa. Kwa hivyo popote ambapo pana hospitali inayoitwa Health Center, magari hayo yarudishwe, yarudishwe na yakae kama sheria na ni sheria.

La tatu ni title deeds; Sasa hivi hapa Mutitu, tunaendelea na mambo ya mashamba na ndio nilikuwa ninataka kuzungumzia ya kwamba yule ambaye atamenyeka kufikia apate huo uwanja ama hiyo shamba, akija kupatiwa title deed, iwe ni forever. Hapana ati kumaliza miaka fulani na iwe sasa si yako tena. Ni forever, hiyo ni yako, kwisha! Hata wajukuu na wajukuu na wajukuu wataikuta ikiwa yako. Hakuna kutolewa pale. Na hata ikipatikana mali hapa chini, itakuwa ni yako, hapana kunyanganywa.

Na nne, chief awe na askari, wezi wamezidi na pengine wamezidi kwa sababu D.O. hana gari ya kuwapeleka Kitui. Wezi wamezidi, na chief hana askari, D.O. hana gari, sasa ukiibiwa mbuzi, ukiibiwa shamba, ukiibiwa nini, unatangatanga hapa na wewe huna mali. Hiyo inapotea unaachilia kwa sababu huyu mtu ni lazima umpeleka wewe kwa tikiti yako, chakula ni yako, ya mahabusu, na ya askari na ya kila kitu. Kwa hivyo chief awe na askari. Kama ni mtu ameiba, akipelekewa repoti, amtume askari atamkamata yule mtu. Na ikiwa D.O. ana gari, huyo atafikishwa Kitui.

La tano ni, vyama. Viwe vitatu tu. Kwa sababu vyama, wengine wanaandikisha chama kikisajiliwa baada ya uchaguzi, kwa sababu wanajua watakuja kupatiwa kitu na Serikali, hata kama chama chake kikuanguka, hakitapeleka mjumbe bunge, mwenyewe amenyakua pesa na amekwenda nyumbani. Kwa hivyo, vyama vikae vitatu. Hiyo inatosha. Kwa nini viwe mingi hivyo?

La sita ni kiapo kwa askari. Wakati askari wakimaliza masomo yao Kiganjo, siku ile watatoka pale, kiapo chenyewe kwa ajili ya rushwa, alishwe kiapo. Kama ni Mkamba, alishwe kiapo cha mbuzi, kama ni kabila nyingine vivyo hivyo. Mimi ninajua kila kabila huku Kenya inakiapo chake, alishwe hapo hapo kwa sababu tumechoka na corruption. Akija kupokea bribes anakufa. Kwa hivyo, hiyo ningependelea iandikwe kama sheria. Asanteni sana, hayo ndiyo yalikuwa maoni yangu kwa sababu tangu nianze kusikiliza, sikuyasikia yakitajwa. Asante sana.

Com Wambua: Asante sana Bwana Mwakavi, tafadhali jiandikishe hapo. Sasa ningependa kuwajulisha kwamba tumefikia mwisho wa kikao hiki, huyo ndiye alikuwa wa mwisho kuzungumuza kulingana na orodha ambayo tulipewa hapa. Kwa hivyo, ningelipenda tufanye tu vile tulivyo fanya huko Kitui Central, Chairman ama coordinator wa 3C's yuko wapi? Kazi hapa ilikuwa nzuri na tunataka utuonyeshe hawa mliofanya kazi pamoja kama wako hapa wanakamati wa 3C's, tuwajue.

Chairperson 3C's, Rev Kilumi: Wako watatu tu ambao wako hapa. Tuko na Celestina, Amolo na Mheshimiwa, mimi na Coordinator, ambao tuko hapa. Wale wengine tutakutana kesho, wako huko (?) tutakutana huko.

Com Wambua: Vizuri, sisi tumefurahia kazi ambayo imefanywa hapa Ndoa, kwa maana hata Kizungu, kidogo wametushinda pande hii. Lakini, maoni tumeyapokea na kunaonekana kulikuwa na matayarisho ya kutosha. Kwa hivyo, kwa niaba ya Commission, Com Dr Mosonik, Com Riunga Raiji, ningependa kuwashukuru nyote kwa mipango ambayo ilipangwa na maoni ambayo mmetoa. Maoni yote tutayapeleka kule ofisini Nairobi. Tukimaliza kuyapokea maoni yenu, kawaida tutayarisha report ambayo tutarudisha hapa, hapa kisheria. Sheria inasema tuje hapa na hiyo report. Report mutaichunguza muhakikishe ya kwamba, maneno yote na maoni yote ambayo mliyoyatoa yako kwa report. Na kama kutakuwa na recommendations zingine kutoka kwenu, basi tutazipokea tena. Kwa hivyo hatujamalizana nanyi, tutarudi hapa hapa tena. Mwishowe, tukishakubaliana na hiyo report, basi hiyo draft Bill ama draft Constitution, tutaiandika na tuipeleke bunge halafu itapitishwa kawaida.

Kwa hivyo, ningependa kuwashukuru nyote kwa kazi njema. Pia ningependa kumshukuru Bwana D.O. ambaye ameketi nasi tangu asubuhi, alitupokea hapa, hata alifika mapema kutuliko sisi. Na sehemu hii ya Kitui, provincial administration imetusaidia, imesaidia Commission, hiyo ni fact. Hata coordinator hapa anasaidiwa sana kupitia kwa ofisi ya D.C., kwa hivyo tunataka kumshukuru bwana D.O. kwa kazi yake njema pia na generally the provincial administration kwa maana wamesaidia. Kwa hivyo ningependa kufika hapo na sijui kama tulianza na maombi?

Response from the audience: Ndio.

Com Wambua: Basi lazima tumalize na maombi. Nilisikia kuna Reverend pahali, yuko bado? Hata moja yuko hapa, kwa hivyo huyo ndiye atatuomba, lakini kabla ya hayo, Bwana D.O. ulitukaribisha hapa kwako, tafadhali utazungumza kidogo, utupatie nafasi ya kuondoka, vile, vile mlifanya na Mheshimiwa, mtupatie nafasi ndio tufunge kikao rasmi halafu tuondoke.

D.O.: Thank you very much Com Musili na Commissioners wenzako, MP, Coordinators, na wananchi wote wa Mutitu. Nafikiri tumekaa kwa muda mrefu kwa hiki kiti na imefaa sana, sana, sana. Ninasema nyote mjue kwamba, ni shukurani, (?)kwa sababu mumechangia na hiyo ndio (?) ametupatia. I am very sure Bwana Commissioners mukienda huko juu (?) because we have done our best. Kwa hivyo ninawatakia safari njema na murudi tena wakati mwingine.

(Clapping from the audience)

Hon Kitonga: Nadhania nitasema machache, na yangu ni kusema kwa niaba ya watu wa Mutitu Constituency. Sisi tumesema shukurani sana, kwa kuja kwenu kuyachukua maoni yetu, hakuna yeyote atakayeenda akilalamika ati alikuwako na maoni na hakupatiwa nafasi. Kila mtu amepatiwa nafasi, amesikilizwa sasa mtu akisema maneno yake kule sokoni, yeye ndiye anajua. Nafasi ilikuweco hapa, na ilikuwa hadharani na ilikuwa mchana, kile kiko tu ningependa kuwa uliza nyinyi Commission kitu kimoja. Please, do your work honestly, for the betterment of your country. isije ikawa haya maoni yote tunafanya, labda kuna Katiba nyingine imefichwa pahali, iwe tu munachukua maoni yetu lakini kumefichwa Katiba. Be honest to your work and God will help you. Thank you.

(Clapping from the audience)

Com Wambua: Nafikiria lazima nitaje kitu kimoja kwa maana Mheshimiwa ametoa maoni kidogo. Sisi kama Tume, tunafanya kazi yetu kwa uaminifu na kwa kweli mkiangalia vile tumefanya kazi hapa, hakuna kazi ambayo tumefanya chini chini. Maoni yenu yamekuwa recorded na yako hapa kwa mitambo, na tumechukua kiapo, and I talk on behalf of all Commissioners. Na nimi nimefanya kazi nao karibu miaka miwili sasa na hakuna Commissioner kati ya wale wako hapo nafikiri anaweza kukubali kuwa ati, ataleta Katiba ambayo iliandikwa zamani na ndio tulete, tuseme ni ya wananchi, hakuna. Ninaweza kusema hayo, nikisema hayo ninasema on behalf of the other Commissioners.

Kwa hivyo, muwe na hakika ya kwamba maoni ambayo mmeyatoa yataingia kwa report, na ndio tunasema tutaleta hiyo report hapa muichunguze kweli muhakikishe yes, hivi ndivyo tulivyosema. Na kama mnasema kuna maneno ambayo yameongezwa ama yameachwa, tutakuja hapa msemi haya hayako, halafu tutaenda tuyaandike hayo tena. Kwa hivyo hiyo ni hakikisho tunataka kuwapatia. Hiyo haitakuwa kama ni kazi bure, lazima itazaa matunda na muwe na hakika mtapata Katiba ambayo iko na maoni yenu.

Kwa hivyo Bwana Mheshimiwa, I am telling you on behalf of the Commission and the Commissioners that we do not have a draft Constitution. I know there is a lot of talk of draft Constitutions existing... we do not have a document of that caliber, in fact as I talk to you now, there are people analyzing views which we have already collected from other provinces, in Nairobi, not even the Commissioners, analyzing and categorizing them. And we are yet to see it and I don't think any of the Commissioners will accept that arrangement where we come with a draft Constitution. And if it were there, we would have circulated it, so that you can give us views on it. So, if we have not given it, it is not there. So, kama wenzangu wanataka kuongezea kitu niwape nafasi halafu tufunge kikao rasmi.

Com Raiji: Just to say that, nimeshukuru sana. Nilikuwa hapa hivi karibuni, tumekaribishwa vilivyo na tumeona Mheshimiwa na kamati ya hapa na Bwana D.O. wamefanya kazi nzuri, nimesema asante sana.

Com Mosonik: Na mimi niseme kwamba, kama Commissioner, nimefurahi kuwatembelea. Sisi husikia kwa radio tu kuhusu Ukambani hasa sehemu hii. Mmesikia mimi nimetoka pande za Rift Valley, sehemu za Bomet, pengine wengi wenye hamjafika kwetu lakini sisi wote tuliteuliwa kuwafanyia kazi. Na tukiwa pamoja vile tuko, tuko kama balance, mnajua. Watu wengi hapa wamependekeza kwamba kuwe na checks and balances. Tuseme ofisi ya Rais iwe ina chekiwa na bunge na bunge i-check korti na vitu kama hivyo.

Tukiwa kwa tume hii yetu, tumechanganyika kabisa, mchanganyiko maalum wa Wakenya wote. Commissioner huyu ni wa Eastern province lakini yeye ametoka Meru, huyu ni wa Eastern province, ametoka sehemu hii, wako wa Rift Valley, wako Waislamu, WaKristo, wanaume kwa wanawake, sisi ni mchanganyiko maalum, ule wa Kenya ambayo tunataka, ile iko mbele. Na ningependa kuwahakikishia kwamba, tutafanya vile tulikula kile kiapo, ambacho mzee amekitaja hapa, sisi tulikula hicho tayari, asanteni sana.

(Clapping from the audience)

Com Wambua: Kwa hivyo Bwana Chairman, pia reverend, unaweza sasa kutuombea ndio tufunge kikao, halafu tutakutana tena. Endelea.

Rev Kiluni: Asante. Kabla ya kuomba ningesema hata sisi watu wa 3C's, the members, tumeshukuru sana, watu wa Mutitu. Hii ni Location ya Mutitu, maCommissioners, wamekuja kwa wingi vile mnavyo ona na sisi tunashukuru sana kwa kuwa mmekuja. Hata hatukufikiri mngefika kwa wingi hivyo. Kwa hivyo Bwana D.O., Mheshimiwa na wale wengine ambao tumesaidiana, na wale wengine wa Civic education providers, mmetufanyia vizuri sana, na mmetusaidia sisi watu wa 3C's, hatungefanya hiyo peke yetu. Hata yale tumepata leo, Commissioners, hatungefikiria kama ingetoka, lakini hata sisi tumekuwa na moyo sana na tumesikia furaha nyingi sana. Kwa hivyo, watu wa Mutitu kama vile mmekuja nafikiri tutajenga hii

constituency kwa moyo huo mmoja na Mungu awabariki sana, tuombe.

Prayers: Baba tunakushukuru sana, Mwenyezi Mungu kwa ajili wewe ni Mungu, na kwa ajili ya wakati umetupatia kuwa pamoja, Bwana tunakushukuru sana. Tena tunashukurani nyingi kwa ajili ya kutupatia maCommissioners, kwa ajili ya uongozi ambao Bwana tunategemea na tunaongojea ili vile tutaendesha hii Kenya yetu. Na tunaizungumzia siku hii ya leo, na tutaendelea kuzungumzia. Tunawaomba maCommissioners wetu, Bwana ukawaongoze ndivyo wakatutolee mambo mazuri ambayo yanaweza kutuongoza katika nchi hii yetu. Na sisi pamoja Bwana tukiungana ukawe pamoja nasi. Neema na utukufu, na rehema zako Bwana zikatulinde na zikawe pamoja nasi. Na ni katika jina la Yesu Kristo tunaomba, Amen.

Meeting ended at 5.30 p.m.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&